The Assistant Minister for Agriculture, Livestock Development and Marketing (Dr. Misoi): Mr. Deputy Speaker, Sir, I beg to reply.

(a) Yes, I am aware.

(b) The NCPB normally has a storage capacity of 30.9 million bags. At the moment, the stock in the stores amounts to about 8.5 million bags. There is therefore adequate storage capacity in the Board's network to take in grain.

(c) The Government is aware of the difficulties that have faced farmers during the transitional stages of cereal markets liberalisation. It is for this reason that a variable duty was introduced. As stated by the Minister for Finance during the Budget presentation, this has now been enhanced and is expected to be effective. In addition, an *ad vorem* tax has been introduced on cereals products imported into the country to help reduce would-be-dumping.

(d) With the advent of liberalisation of the grain sub-sector, farmers are now at liberty to sell their cereals to buyers of their choice. Indeed, a number of wheat farmers have already entered into contractual arrangements with millers who buy their produce directly. However, as explained above, the Government has introduced these measures on imported cereals which will help curb dumping. My Ministry will continue to monitor the situation and will take appropriate measures should there be excess grain in the market; by using the NCPB to receive surplus grain from the farmers.

Mr. Rotino: Mr. Deputy Speaker, Sir, I just want to inform the Assistant Minister about what he does not know. He is aware that the National Cereals and Produce Board (NCPB) has subjected farmers to untold suffering by not paying them for their produce. Could he, therefore, tell this House the date on which the Government is going to pay farmers to the tune of Kshs2.2 billion which is still unpaid?

Dr. Misoi: Mr. Deputy Speaker, Sir, the Government is doing all it can to ensure that farmers are paid for produce delivered. So far the Government has done very well and it will continue doing so in the future.

Mr. Kirwa: Mr. Deputy Speaker, Sir, taking into consideration the fact that Kshs2.2 billion is yet to be paid to farmers and further considering the fact that maize has started being harvested in the areas the hon. Member has mentioned in his Question, and knowing that the Government does not have this amount of money - otherwise it would have paid the farmers - what measures will the Assistant Minister put in place to ensure that farmers will be paid the balance of last year's crop at the time of their being paid for the crop that is going to be delivered soon?

Dr. Misoi: Mr. Deputy Speaker, Sir, the NCPB has been paying farmers for the maize delivered to date.

The Government, through the NCPB, will continue doing so until the balance is finally paid. Secondly, the Ministry has assured this House that measures will be put in place to ensure that surplus maize produced by the farmers will be received by the NCPB.

Dr. Kituyi: Mr. Deputy Speaker, Sir, it is sad that an Assistant Minister is misleading this House by pretending that the Government is making any attempts to pay farmers the outstanding money for last year's crop when there is no policy whatsoever to guarantee farmers that there is going to be any payment to them for this year's crop! There is no minimum price promised for the first time since Independence! Be that as it may, considering that when the Government noticed that anti-dumping measures were not sufficient to stop the greedy from importing cereals into this country, it imposed a temporary ban on importation of cereals. However, since the publication of Legal Notice No.216 of 15.6.95 by the Minister for Agriculture, Livestock Development and

Marketing, there has been a flood of cereals into this country.

So, could this Assistant Minister tell the House what specific anti-grain importation measures are possible short of banning the importation again, so as to stop this importation by powerful people including, as I showed last week, Ms Jusung Enterprises of Bawazir and hon. Sajjad?

Dr. Misoi: Mr. Deputy Speaker, Sir, indeed, the Government is very serious about this matter. The measures which I have outlined are expected to be effectively implemented so as to reduce or stop excessive importation of grain into this country.

SALE OF BIXA COMPANY

Mr. Mwavumo: Mr. Deputy Speaker, Sir, I beg to ask the Minister for Finance the following Question by Private Notice.

(a) Is the Minister aware that Bixa Company Ltd. in Kwale District, is being sold without public advertisements as required by the financial regulations and also without independent valuation?

(b) Since Bixa Company Ltd. is among the few parastatals that pay dividends to the Treasury, why is it being sold to foreigners?

(c) What urgent steps is the Minister taking to stop the purported sale and ensure that if the company is to be sold, only the indigenous people from Coast Province will be allowed to buy it?

The Assistant Minister for Finance (Mr. Keah): Mr. Deputy Speaker, Sir, I beg to reply.

(a) Yes, I am aware that Bixa Company Ltd. was sold without public advertisements. Since the company was privatised through the pre-emptive rights it required no public advertisements.

(b) Four independent valuations were done by Ms Price Waterhouse, Githongo and Company, PMG Peat Marwick and the management of the Kenya Bixa Company Ltd. itself. I am not aware that Bixa Company Ltd. was sold to foreigners at a throw-away price. However, I am aware that it was sold at the highest valuation price.

(c) The final transactions were completed in May, 1995 and, therefore, the question of stopping the sale does not arise.

Mr. Mwavumo: Mr. Deputy Speaker, Sir, what was the purpose of selling off the only processing company in Kwale District?

Mr. Keah: Mr. Deputy Speaker, Sir, as you are aware, in the privatisation programme the Government is disposing off all the non-strategic State Corporations. The Bixa Company Ltd. is not one of those strategic corporations. Therefore, this is the reason why it had to be sold.

Mr. Kiliku: Mr. Deputy Speaker, Sir, the Kenya Cashew Nuts Company was sold under the same arrangements of the Ministry. The Assistant Minister said Kenya Bixa Company Ltd. was sold for the highest price. How much was that highest price?

Mr. Keah: Mr. Deputy Speaker, Sir, the valuations were as follows: Price Waterhouse Kshs125.00 per share; Githongo and Company Kshs658.00 per share; KPMG Peat Marwick Kshs472.00 per share and the Kenya Bixa Company Ltd. Management Kshs698.00 per share. So, the company's total shares of 100,000 ordinary shares were sold at the highest price of Kshs698.00 per share.

Mr. Gatabaki: On a point of order, Mr. Deputy Speaker, Sir. Is it in order for the Assistant Minister to mislead the House while knowing very well that there was no formula whatsoever for selling this company and that the company was given out to politically correct individuals?

Mr. Keah: Mr. Speaker, Sir, there is absolutely no truth in what the hon. Member is alluding to. There was a formula, which was that the shares were sold on the basis of pre-emptive rights provided for in the Companies Act!

BILL

Second Reading

THE FINANCE BILL

*(The Assistant Minister for Finance
(Mr. Koeh) on 6.7.95)*

(Resumption of Debate interrupted on 6.7.95)

Mr. Shikuku: Bw. Naibu Spika, tulipolarisha Bunge hili siku ya Alhamisi, mhe. Dalmas Otieno aliwahi kuuliza kama thibitisho linaweza kutolewa kwamba kuna ufisadi na usimamizi mmbaya katika Wizara yake, na hii ndiyo ilifanya Shirika la Ndege la Kenya kupata hasara ya Ksh.6.7 bilion, ambayo sasa anataka iwekwe kwa watoa kodi wa nchi hii. Wakati huo, nilimwambia kwamba ni jambo linalojulikana wazi kwamba kuna ufisadi. Wengine wetu tukisema juu ya ufisadi, tunajua tunasema nini. Hati iko hapa ambayo inaonyesha wazi. Hati hii inaitwa "Kenya Airways and Subsidiaries Directors Report and Accounts dated March, 1994". Sina haja ya kuingilia mambo hayo kwa sababu ni mengi sana, lakini watu wakitaka ukweli na hawataki kusoma, tutawasomesha. Pia, kuna ile hati nyingine ya "Kenya Airways Limited and Subsidiaries Directors Report and Accounts". Ile ya kwanza ilikuwa "draft", sasa hii imetiwa sahihi na Bw. Ndegwa ambaye ni Director na Mzungu mwingine hapa, na inaonyesha wazi kwamba kulikuwako na ufisadi ambao umeleta hasara ya Kshs bilioni 5.3, na hiki kiasi cha pesa kimekuwa mpaka kufikia karibu shilingi bilioni nane.

(Mr. Shikuku laid the documents on the Table)

Mimi ninawashukuru waandishi wa magazeti, hasa, gazeti la *Daily Nation* ambalo lilichora "cartoon" ya ndege ya Kenya Airways ikiwa karibu kuondoka, na huku mzigo mkubwa umewekelewa mwananchi ambaye amekonda sana. Hiyo inatoshia, hata hakuna haja ya kutoa hotuba. Ukiangalia hiyo cartoon, utajua vile mwananchi wa Kenya anavyofanywa. Mwananchi mdogo anafinywa, hata afadhali Mbeberu. Ukweli uko hapa.

Mr. Nthenge: On a point of order, Mr. Deputy Speaker, Sir. The Chamber is too cold for most of us. Can the Chair order that the temperature becomes normal?

(Laughter)

Mr. Obwocha: On a point of information, Mr. Deputy Speaker, Sir. Thank you, hon. Shikuku. From the accounts that have been laid on this Table, the accumulated loss for Kenya Airways as at 31st March, 1993 was Kshs6.064 billion. The following year which is 31st March, 1994, the accumulated loss had risen to Kshs8.09 billion. Now, that is an accumulation of Kshs2 billion in one year. How, then, does the management justify a Kshs2 billion increase within one year, on accumulated losses?

The Minister for Transport and Communications (Mr. Otieno): On a point of order, Mr. Deputy Speaker, Sir. I can accept hon. Shikuku to misread accounts, but I cannot excuse hon. Obwocha to deliberately misread accounts when the hon. Member for Butere tabled all the documents, including the notes to those accounts. Now, Kshs1.6 billion of that increase was exchange losses, and I expected hon. Obwocha, at least, to take note of that before he raised his question. But I am waiting for more questions.

Mr. Obwocha: On a point of information, Mr. Deputy Speaker, Sir. I am not misreading the accounts because, the Minister is explaining how the loss came about---

Mr. Deputy Speaker: Order, Mr. Obwocha! It really is not a point of information any more. You are now hijacking the debate.

Mr. Shikuku: Bw. Naibu Spika, mimi nipewa habari na msheshimiwa Obwocha, na kufatana na haya yote, hata ikiwa hiyo hasara ni kwa sababu ya "exchange losses", mzigo umeshapigwa picha kwa *Daily Nation*, na umewekelewa mwananchi asiye na kazi, asiyeweza kula chakula mara tatu kwa siku, asiyeweza kusomesha mtoto, asiye---! Haya ndiyo mambo tunayosema. Mzigo huu umeletwa na nani? Umeletwa na wakubwa ambao wamenyonya shirika hili mpaka likafilisika. Sasa hasara hiyo inawekewa mtoa kodi. Hilo ndilo jambo mimi ninakataa! Niliulizwa kama kuna ufisadi. Ufisadi uko, na hii ni Ripoti ya Public Investments Committee ya 1993. Ukiangalia ukurasa wa 78, kuanzia pale juu kuna orodha ya ploti ambazo zimeuzwa kwa shirika la NSSF kwa bei ya juu, na wameiba Ksh86 billion, na hii ni kodi ya wafanyakazi. Wananchi wanafanya kazi, huku wakokwa na jasho, na pesa zao zinaliwa hapa na Kanyingi na Wahindi wake. Kamupuni hii ya Wahindi inaitwa Sawaka Investment. Wakurugenzi wa hii Kampuni ni Bw. H.B. Dawada, P.O. Box, 46385, Nairobi, Bw. N.P. Dawada, P.O. Box, 46385, Nairobi, Bw. F.K. Kanyingi, P.O. Limuru, na Bi. F.W. Kanyingi, P.O. Limuru.

Bw. Naibu Spika, waheshimiwa Wabunge wakisema maneno ambayo yako kwa hati ya umma, kuna wengine ambao hawayasomi; wanashindana, na huku kuna ufisadi. Juzi, Mbunge wa Nakuru Mjini alitonyesha maandiko katika Biblia; Yohana 8:44, ambayo inasema kwamba mkubwa au baba ya waongo ni shetani. Ikiwa waheshimiwa Wabunge wanakataa ukweli, basi, mtu anaweza kufikia uamuzi wa kusema kwamba hawa lazima wawe ni wafuasi wa shetani. Na pengine, akiwaita "devil worshippers", itakuwa aibu. Imekuwaje kwamba Serikali hii ikiambiwa ukweli, inakataa? Ukisema kitu chochote, wanakataa! Tumekwenda kwa Mkuu wa

Polisi, wanasema hakuwapo, na tunajua alikuwapo. Waheshimiwa tuna maana. Maana ya "mhashimiwa" ni mtu ambaye anafwata ukweli; mtu aliyeheshimiwa na wananchi wote. Mtu hawezi kuchaguliwa na bibi yake. Sisi wengine yafaa tuheshimiwe sana kwa sababu tuko "senior" hapa. Mwaka kuja, mwaka nenda, tunarudi. Hatuingii hapa bila kupingwa. Ikiwa tunatoa maoni hapa na hayawezi kuaminiwa na waheshima Wabunge wenzetu, basi Mungu aisaidie nchi hii. Tumechoka kwa sababu tunatoa ukweli na hakuna anayesikia, ni kukana, kukana kila wakati na hali wananchi wanaumia. Hii ni aibu sana. Lakini hao ambao wanapuza tunayoyosema uko wakati ambapo wananchi watawapuza wao. Sitaki kuchukua muda mrefu, thibitisho nimefanya na bado mengine yanakuja. Mhe. Otieno akitaka thibitisho nyingine, mhe. Nyagah aliahidi Bunge hili kutoa thibitisho pia. Sasa hatuna haja ya kuthibitisha zaidi. Mambo yako katika maandishi, tungetaka "Watukufu Mawaziri" wasome.

An hon. Member: Wanapiga kura tu!

Mr. Shikuku: Bw. Naibu Spika, siku ya Alhamisi tulikuwa tumefikia Exemption. Katika Ukurasa wa 199 Clause 6(2) wanasema:-

"The owner or agent of an aircraft or vessel who fails to account for any of the goods deemed to be in the importing aircraft or vessel under Sub-section 1 to the satisfaction of proper officer within such a period, may be prescribed or surcharged further as the proper officer may allow, shall be guilty of an offence".

Bw. Naibu Spika, hapo mnampa mtu mmoja anayeitwa "proper officer" uwezo wote. Yeye binafsi, mtu mmoja, ndiye atasema, "umechelewa" au "hakuchelewa" na hapo ndipo mahali pa mlo. Wakati huu Bunge hili linataka kupitisha sheria ambayo itampa "proper officer" mahali pa kupata chakula chake katika nchi ambayo imelemewa na ufiisadi usio na kifani. Mimi naonelea lazima kuweko na kamati au bodi ya kuangalia mambo kama hayo. Lakini kazi hii ikipewa mtu mmoja, hapo utastaajabu kuyaona mambo yatakayofanyika katika nchi hii. Sisi kama Wabunge wa Bunge hili, tunapitisha sheria kama hii ili tupate pesa za Harambee kutoka hapo. We only hear "I understand you are going for Harambee. I can give you my contribution, but please just consider this case".

Hayo ndiyo yataendelea. Waziri akishapata hiyo hongo, anataka kuwa mgeni wa heshima baada ya kuwaibia wananchi. Anaheshimika namna gani na yeye ni mwizi?

Bw. Naibu Spika katika Clause 7 wanasema:

"Customs and Excise Act is amended by repealing Section 23 and inserting the following:

Where goods reported for discharge as a port or place specially allowed by the proper officer are not duly unloaded and deposited in a transit shed or a custom area, then the master or agent of the aircraft or vessel shall, unless he explains to the satisfaction of the proper officer, be guilty of an offence and shall be liable to pay the duty due thereon."

Sasa huyo officer ni mmoja tu na ukishampiga ngumi na awe ametosheka basi maneno kwisha! Mtu mmoja. How? Na hali tunajua watu wameshatajirika kwa kufanya ufiisadi. Nchi hii imekuwa ni nchi ambayo imeshahalilisha ufiisadi. Ukiuliza watu waseme namna walipata mali ile wanayo, wewe utapingwa. Utapata wafanyakazi wa Serikali ambao wanaweza kumlisha mhe. Otieno kwa mfano, wasomeshe watoto wake na yeye mhe. Otieno alipwe mishahara mpaka afe na hali yeye ni mfanyakazi wa Serikali. The amount of money they have made by looting has made them so rich. Sasa hapa bado tunampa nguvu mtu mmoja. Huyu mtu mmoja akiwa satisfied, basi maneno yanaendelea. Sisi Waheshima Wabunge tunatakiwa tupitishie sheria hii. Hii ndiyo sababu nilisema kwamba Mswada kama huu ikija katika Bunge hili, ndiyo kazi yetu sisi Wabunge. Kazi yetu si kufanya Harambee. Kazi yetu ni kusoma Mswada na kutoa makosa na Waziri kusikia na kurekebisha kwa vile watakaoumia, ni wananchi waliotupigia kura kuja hapa.

Katika Clause 8. (i) (c) states as follows:-

"The proper officer may permit the unloading and delivery to the owner of bullion, currency notes, coin or perishable goods without entry, subject to security being given by the owner to finish the necessary entry within 48 hours of the time of delivery."

Hayo maneno ya entry tuliyakuta katika Public Accounts Committee na pia yameonekana katika Public Investments Committee. Na hali hapa leo tunapitisha sheria kumpa proper officer kuendesha mambo kuhusu entry. Sasa Bunge hili linafanya kazi gani? Are we not giving the proper officer and the owner a blank cheque provided he gives him information within 48 hours? Hii si siri, katika practice itakuwa maneno mengine. Mara ngapi tumeona katika Public Accounts Committee unachukua imprest kwenda Ulaya ambayo unahitajika ukirudi utoe risiti na uregeshe pesa zilizobaki kwa Accounting Officer? Tuna watu waliochukua imprest mwaka wa 1987 na mpaka leo hawajalipa. Mimi najua Kenya hii ikitunza pesa na kodi yake, haina ya kwenda kuomba omba nje. Ubovu ni kwamba tunaiba pesa zetu wenyewe. Tukishaiba, tunaenda kuomba, tena tunapanda ndege first class.

Tangu lini mwombaji akapanda ndege first class? Na tena akienda huko, analala katika Five Star Hotels kama Sheraton na nyingine kubwa kubwa na hali amekwenda kuomba. Mwezi huu tarehe 24 wataenda Paris

wakivalia makoti makubwa, makubwa. Aibu hawana! Na huku wanakula pesa zao wao wenyewe. Mimi nafikiria umefika ambapo donor countries should just refuse to give Kenya money ili tufe hapa ndio tupate akili kwa sababu mtu akipewa pesa kila siku hapati akili. Ukimzoesha mtoto kumpa shilingi kila asubuhi, na humfunzi namna ya kupata hiyo shilingi, ukifa atakuwa mwizi.

An hon. Member: Hii Serikali ni ya wezi!

Mr. Shikuku: Bw. Naibu Spika, nakubaliana na huyo Mbunge anayesema hii Serikali ni ya Wezi. Ni kweli hii Serikali ni ya Wezi.

Bw. Naibu Spika, wao wanataka kwenda kuomba pesa tena kutoka kwa mataifa matajiri na hayo madeni yote tunawaachia watoto wetu na watu maskini ambao hawana matumaini ya kupata kazi. Hao ndio watayalipa hayo madeni. Hii ni Serikali gani, ambayo haijali maslahi ya wananchi? Kazi yao ni kusema "KANU itafanya maendeleo." Tunaambiwa kwamba mtu akikihama chama chake na kujiunga tena na KANU kutakuwa na maendeleo katika sehemu yake na ile hali KANU kimeitawala nchi hii kwa muda wa miaka 32 na hakuna maendeleo yo yote katika nchi hii. Wengine wamedanganyika na kuvihama vyama vyao. Sasa sehemu zao zimekauka; Serikali haina lolote na inaenda kuomba. Huyu mtu anayetajwa kama "proper officer" hapa ana mlo wake. Yeye anauwezo wa kufanya mambo mengi.

Kifungu cha 36 kinasema:-

"Section 19 of the Customs and Excise Act is amended by deleting sub-section one and inserting the following new sub-section:-

"The Minister may by order in the Gazette, amend the First Schedule or the Fifth Schedule by increasing or decreasing any of the rates of import duty, export duty or excise duty by an amount not exceeding 30 per cent of the rate set out therein."

Hapa ndipo Waziri atapata harambee. There should be no taxation without representation. Ni kwa nini hatuwezi kuwa na kamati ya kuyashughulikia mambo haya? Kamati za Bunge hili hazifanyi kazi. Wabunge hawafai kudhani kwamba wanaweza kufanya maendeleo. You cannot develop with your Kshs10,000.00 per month! Yafaa kila Wizara iwe na kamati zake kulingana na Kanuni za Bunge hili. Hii ni kwa sababu Waziri akipewa "kitu kidogo" anaweza kutumia mamlaka yake kwa njia isiyofaa. Ni lazima kuwe na kamati za Bunge za kushughulikia mambo kama haya. Ni lazima Kamati ya Fedha ya Bunge hili ifanye kazi yake.

Wakati mwingine aliyekuwa Mbunge wa Kimilili, mhe. Mwangale, alisema kwamba siku moja fisi alikuwa akienda zake nyumani. Unajua sisi tunapenda kusema "*mirembe*" and this means "peace." Huyu fisi aliliambia jiwe "*mirembe*" lakini jiwe halikujibu. Akasema tena "*mirembe rundi*" lakini jiwe halikujibu. Yule fisi alipoona kwamba hakuna jawabu--- Unajua ukimsalimia mtu halafu akatae kujibu salamu zako utajua mara moja kwamba mtu huyo hataki amani. Basi fisi alipokosa kupata jawabu kutoka kwa jiwe alisema "hata kama hukujibu umesikia" halafu akaenda zake. Sisi tunasema kila wakati lakini hii Serikali yetu "tukutu" na "takatifu" ya KANU haisikii. Lakini hata kama hawajibu tunajua wamesikia. Kuna siku moja ambapo watatoa hesabu juu ya mambo haya yote.

Bw. Naibu Spika, Mswada unaendelea kusema:-

"In case of maize, wheat, sugar, milk rice or used clothing, the rates of duty may be increased by an amount not exceeding 75 per centum of the prescribed rates."

Sehemu hii ya Mswada inanikumbusha jambo ambalo nililitaja hapa na niwasilisha ushahidi hapa lakini ikasema kwamba hizo zikuwa "fake papers." Karatasi zangu zilisema kiasi cha 20,500 metric tonnes, za mahindi ziliagizwa kutoka ng'ambo. Karatasi iliyoletwa hapa baadaye ilisema kwamba walileta kiasi cha tani 10,000 za mahindi. Je, "fake papers" zilitoka wapi? Bw. Spika alisema kwamba atalichunguza jambo hilo na kwa hivyo sitaki kulifuatilia kwa sasa. I am not yet through with that. Hii ni kwa sababu niko na ushahidi mwingine zaidi. Mimi nikianza kukufuata sikuachi; nitakufuata mpaka Yesu arudi.

Bw. Naibu Spika, Waziri anayehusika anaweza kuyazuia mambo haya. Hii ni kwa sababu wakulima wamefilisika. Watoto wao hawasomi. Hata wale walioyapeleka mahindi yao kwa National Cereals and Produce Board mpaka leo hawajalipwa. Nafikiri Serikali hii ina mpango wa kuwafilisisha wananchi ili wawe wapole. Hii ni kwa sababu kama hujiwezi kifedha, wewe ni mtu wa kutii amri. Kuna mpango katika Serikali hii wa kufanya maskini watu wa nchi hii ili waweze kunyanyaswa na matajiri. Huu ni mpango sawa na ule wa aliyekuwa dikteta huko Romania lakini leo yeye hayuko. Wakijua kwamba wanaweza kupata faida kutokana na mbuzi wako, mbuzi hao wataibwa. Ninavyozungumza sasa hivi, katika Mawakilisho ya Butere na mahali kwingineko, mifugo inaibwa na haipatikani. Hata wanatumia malori kubeba mifugo iliyoibwa. Ukiuliza Chifu, DO, au DC hawataki kukwambia mambo yako namna gani. Sisi watu wa Butere tunajua kwamba machifu wakikamatwa na kutiwa korokoroni hiyo itawaamsha kidogo. Lakini hawawezi kufanya hivyo. Hii ni kwa sababu mali hii ya watu inayoporwa inagawanywa kuanzia kwa chifu, DO, DC hadi juu. Hawataki kuchukua hatua yo yote kwa sababu wakifanya hivyo wizi utakwisha na wao hawatakuwa na mahali pa kupata chakula.

Kitu wanachotaka ni *chang'aa*. Ukiwaambia kwamb kuna pombe ya *chang'aa* mahali fulani wanatoka na bunduki lakini ukiwaambia kwamba ng'ombe wameibwa hawataka kuwafuata hao wezi. Hii ndiyo Serikali ya KANU; yenye maendeleo! Watu wataendelea namna gani ikiwa mifugo yao inaibwa? Kule Marakwet watu wanafilisishwa sasa. Hawana cho chote isipokuwa mbuzi na ng'ombe; hawana hata barabara. Kama kuna Serikali mbovu zaidi ya nyingine katika bara la Afrika, hii inaweza kushinda kikombe cha ubovu.

Utaona kwamba katika nchi kama Amerika, mkulima huwa ana hakika kwamba hata kama mazao yake hayanutuliwi atalipwa na Serikali hiyo; Serikali yao inayachukua hayo mahindi ya kukitoa kama misaada kwa mataifa mengine au kuyamwaga ndani ya bahari ili samaki wale na kuzaana.

Lakini Serikali yetu hii haipunguzi bei hata nimeangalia hapa na bei ya mbolea hawapunguzi. Mwananchi ananunua of DAP kwa Kshs1,300 anatia ammonia Kshs.1,000, anaweka mbegu Kshs3,000 na sasa unapewa na Waziri wa Kilimo Ksh400 au Ksh500 kwa kila gunia. Hata kama hujui hesabu Bw. Naibu Spika, wewe umetumia Ksh3,000 lakini unapatiwa Ksh500.

The Minister for Agriculture, Livestock Development and Marketing (Mr. Nyachae): On a point of order Mr. Deputy Speaker, Sir. The Minister for Agriculture, Livestock Development and Marketing has never paid any farmer Kshs400. For the information of the hon. Member, the minimum price that National Cereals and Produce Board (NCPB), which comes under the Ministry of Agriculture, Livestock Development and Marketing, is Kshs900 and not Kshs400.

Mr. Shikuku: Bw. Naibu Spika wa Muda, mimi nasema yale ninajua. Hapo mbeleni mahindi yalikuwa yakinunuliwa kwa Ksh400, ikafikia Ksh500 na baadaye ikafika Ksh600. Hata kama hujui hesabu, umetumia Ksh1,300 kununua DAP na Ammonia, mbegu Ksh700; wacha kulima, kupalilia na kuvuna. Bado unalipwa Ksh900 kwa gunia hii ambayo anasema hapa Bungeni. Hesabu ikitofautiana si mkulima anaungua?

The Minister for Agriculture, Livestock Development and Marketing (Mr. Nyachae): On a point of order, Mr. Deputy Speaker, Sir. The calculation the hon. Member is giving is misleading. The actual cost of production is not what he is stating. The hon. Member is misleading the House. If he is misleading the House he has to be corrected. The maximum cost of production per bag of maize has never exceeded Kshs.758, and we are paying Shs.900 minimum.

Mr. Shikuku: Bw Naibu Spika, nikamaliza umpe nafasi Mhe. ajibu. Nataka kumfundisha kanuni za Bunge. Ikiwa hakubaliani na mimi anukuu yale ninayoyasema na nikishamaliza mpe nafasi aeleza yake. Lakini tukianda naye kwa wakulima hatasema yeye; anasema hapa tu! Aende kwa wakulima wamwambie maneno. Hili ndiyo sababu anatembea na askari wa kuwalinda. Mimi sina haja ya askari wa kunilinda. Kwa vile wanawaumiza raia inawalazimu kutembea na askari wa kuwalinda, tena wenye silaha!

Bw. Naibu wa Spika wa Muda, ukweli ni kwamba wakulima katika nchi hii, wawe wa KANU au wawe Upinzani, wanajua ninayosema ni kweli. Hakuna mkulima ambaye amefurahi. Tunaumia. Wakulima hawajalipwa hata hiyo Ksh900 hadi sasa. Lakini yeye hahisi uchungu. Yeye ni Waziri! Nao watu wanaosaga mahindi, wanunua gunia la kilo 90 na kutengeneza pakiti ya jogoo kuiuza kwa Ksh45! Kwa gunia moja anapata Kshs.2,500. Na mkulima anapewa Kshs.900 na Waziri anacheka! Sasa hiyo ni haki? hata wabeberu hawakufanya hivyo. Watu wa kawaida wananyanyaswa na matajiri.

Katika mataifa ambayo yameendelea, ikiwa wewe ni Waziri na unahusika na biashara inayohusiana na Wizara yako, basi huhitaji kuwa Waziri katika Wizara hiyo ambayo ina mambo ya biashara ya aina hiyo. Lakini hapa Kenya, unawekwa mahali pa kutafuta Harambee.

Pia mambo ya sukari yako hapa. Kuhusu sukari, tulikuwa karibu kulisheleza taifa hili. Nzoia Sugar Company ilivurugwa. Ilivurugwa na wanasiasa wa wakati huu, mhe. Mwangale na wengine. Ukienda kule Ramisi, Sondu na kwingineko, wahindi wameharibu.

Kenya inaweza kuwapa watu wetu kazi. Kilimo cha sukari, mahindi na pia mchele wa Mwea kikiangaliwa sawa kinaweza kutoa kazi kwa watu wetu na kutoa chakula cha kutosha. Lakini wakubwa ndio wanaoagiza vyakula kutoka nje kumwumiza huyu mwananchi. Hana matumaini!

Miwa katika Butere inatoa maua. Na miwa inapotoa maua haina uzito. Na mkulima amengojea miezi 18 hadi 30 ili akate miwa yake kwa sababu wakubwa wameagiza sukari kutoka nchi. Ni lazima uwe mkubwa na uwe na marafiki wa wakubwa. Hii ni njia moja ya kuua wakulima wa Kenya. Hii ni njia moja ya kuwaua watu wetu wa Butere na Mumias na wale wengine wa mhe. Ommani na hata kule kwa mhe. Sifuna. Hawa ndio watu ambao wanataka kupata riziki zao kwa sukari. Lakini hawawezi kupata kwa sababu sukari imeagizwa kutoka nje na bei ya sukari ikaongezwa. Hapo tunampa mkubwa uwezo kwa upande wa sukari, maziwa, mchele na ngano.

Bw. Naibu Spika tunapitisha sheria hapa kumpa nguvu tena na sisi tunaweza kujitegemea hata katika ngano. Wakati umefika Waziri wa Kilimo alete hapa Mswada wa kusema kwamba kuna sehemu maalum za pareto, ngano, mahindi, kwa sababu ukitoka Nakuru ukielekea Eldoret hapo zamani sehemu hiyo ilijaa ngano. Ukitaka kuona vizuri chukua ile njia ya Kabarak. Zamani sehemu hiyo yote, hadi mahali Hayati Kenyatta alikuwa

na shamba, kulikuwa ngano. Lakini siku hizi watu wanajaribu kupanda mahindi, lakini mahindi hayastawi vizuri katika sehemu hiyo.

Kwa hivyo, Bw. Naibu Spika, tunahitajika kuzalisha vyakula katika nchi hii. Tunataka sheria iletwea hapa ya kugawanya sehemu hizi. Mtu ambae ni mkulima wa ngano alime ngano, natupate ngano nyingi zaidi. Wengine wanajaribu kupanda mahindi na hata saa ile unapita njia ya kwenda Kisumu ukielekea Eldoret, ukienda kule ng'ambo wanajaribu kupanda mahindi. Lakini hayawezi kukuwa kwa sababu kuna baridi sana, inahitaji ngano na pareto. "This is waste of strength, time and yielding nothing". Waziri yafaa aangalie hiyo, lakini hawataki hiyo kwa sababu wanataka kuleta bidhaa kutoka nchi nyingine ili wapate pesa. Lakini hawataki kutajirisha mtu wa Kenya, wanataka wao ndiyo wawe tajiri, ndiyo wawe wakitowa Harambee. "Hatutaki maneno tunataka vitendo." Vitendo vya wizi, wanaambia wananchi halafu wanawaambia harambee ndiyo hii. Iko siku watagundua na yale mambo yaliyowapata Wafaransa itakuwa afadhali. Mtakwenda mbio na hizo mtokaa zenu, lakini mutaona. Hatuwezi kuendelea namna hii milele na milele, watu wananyanyazwa.

Bw. Naibu Spika, tuna hii Mwea-Tebere na hata ile ya Kisumu - Nyando, zipandwe ngano, watu wapewe mkopo waendeshe kilimo yale maji yanawaua wakwe zangu kila siku mvua ikinyesha yatumike. Mto unachukua kuku wote kwa sababu kuku hajui kuogelea. Katika sehemu hizo tunaweza kutengeneza bomba la kuzuia maji ili wale watu waendele kupanda mpunga na wakifanya hivyo tutakuwa na mpunga kwa wingi.

Wao ndiyo watakuwa wakitoa Harambee. Hatutaki maneno. Tunataka vitendo. Hivyo ni vitendo vya wizi wa kuimbia wananchi, halafu tunaambiwa Harambee ndiyo hii. Iko siku watagudua. Yale mambo yaliyowapata Wafaransa yatakuwa afadhali. Mtakwenda mbio na hizo motokaa zenu na mtapata taabu. We cannot go on for ever like this being exploited.

Bw. Naibu Spika, tuko na Mwea Tabere, na hata ile ya Kisumu, Nyando. Inafaa watu wapewe mkopo waendeshe. Na yale maji ambayo yanauwa wakwe wangu kila siku mvua ikinyesha - mtu anabeba kuku zake kwa sababu hawajui kuogelea - tunaweza kutengeneza dam ili wale watu waendele kupanda mpunga kwa wingi.

Bw. Naibu Spika, hapa ulisikia zile nguo kuu kuu kwa hiyo Clause ambayo natoka. Hizi nguo zinasaidia wananchi, wale ambao hawajiwezi. Kama zingekuwako, wananchi wengi wangukuwa wanatembea uchi. Lakini ni nani ambaye analeta hizi nguo kuu kuu? Mbona yeye anakuwa exempted from paying the tax? Mhe. G.G. kariuki anauliza ni nani huyo. Unajidai hujui. Pengine nikwambie it is the son of the tall ones. Wewe ukileta, utaona cha mtema kuni kwa sababu wewe ni mfupi. Lakini nguo kuu kuu zinaletwa na hawalipi kodi. Why? Hawa ni watu wakubwa. They should be dismissed for siphoning all the money outside.

Bw. Naibu Spika, wacha nije kwa jambo la ukurasa wa 204, Clause 37. Nataka kwenda haraka. Sisi wengine husoma hizi vitu sana, na ndiyo unaona tunazungumza kwa muda mrefu. Hii ndiyo kazi nilichaguliwa kuja kufanya hapa. Sikuchaguliwa niwe nikitoa Harambee. Jambo ambalo nataka usikie ni hili:

"Provided where the maize, wheat, sugar, milk, rice, textiles, new and used clothing and footwear are imported during the periods of civil strife, national calamity or disaster declared under any law for the time being in force or where they are intended for use in officially recognised refugee camps in Kenya, duty in respect thereof may be remitted under this section."

Bw. Naibu Spika, kuhusu calamity hapa kwetu, Mungu ametubariki hatuna nyingi, lakini vitu hivi vyote bado vinaingia. Hata kuhusu mahindi, wengine wanasema, wakati Value Added Tax (VAT) ilikuwa waived, iliingia. Inaumiza nani? Mwananchi mdogo. Calamity is something real, na pia tumesema kwamba tukiweza kutoa chakula au wakulima wakiwa subsidised in all agricultural inputs, tunaweza kutoa chakula cha kutosha kuwekwa tukingonjea calamity, na disaster. We can do that. Siyo kungojea ikuje ndiyo tufanye Harambee. Bona hatujiweki tayari na tuko na chakula kingi katika Kenya hii, kama Serikali inaweza kununua chakula na kukiweka katika ghala ikingojea calamity. Hata hivyo, inafaa wafanye huo mpango kwa sababu watu wa Ukambani kila mwaka wanasaidiwa. Ukambani is a permanent market. Kwa nini wasitengeneze mpango tuweke chakula cha kutosha wakati wa calamity, taking into account Ukambani area ambapo wamekataa kuwapa maji. Kila mwaka wanapewa msaada ndipo kura ipatikane. Wakamba mko na taabu lakini waheshimiwa Wabunge wenu hapa, saa nyingine wanastua sana. Hawasemi mambo ya maji ya Ukambani.

[The Deputy Speaker left the Chair]

*[The Temporary Deputy Speaker
(Mr. Wetangula) took the Chair]*

An hon. Member: Hakuna maji huko?

Mr. Shikuku: Mhe. Mbunge mmoja kutoka Turkana aliniuliza, "Kwani huko Ukambani hakuna maji?" Hana habari Ukambani iko wapi. Kwanza kule Turkana ndipo kuna shida zaidi kuliko Ukambani. Nyasi

hakuna kule Turkana. Kuona maji ni kama kuona almasi. Mhe. G.G. Kariuki hapa anafahamu yale ninayosema. He is nodding in agreement that it is difficult to see a green blade in that area. Hayo mambo ndiyo ambayo mimi ninazungumza. Mimi ni Mbunge na kila mhe. Mbunge mwingine hapa ni wa National Assembly na ana kazi ya kuangalia Kenya yote kwa sababu wananchi wote ni wetu. Akiwa wa KANU au wa Upinzani ni mwananchi. Hata akiwa Mturkana, Pokomo, au kutoka Butere, yeye ni mwana Kenya. Hii ndilo jambo ni heri Waheshimiwa Wabunge wanatakiwa wajue, kwamba wanapata taabu. Ni wajibu wetu wote katika Bunge hili, kwa sababu wengine wanaambiwa waingie kwa chama cha KANU. Hata ukiwa kwa KANU, ukienda ndukani, ukitingiza kidole, bei hairudi chini. Ile bei Mpinzani anapata ndiyo hiyo hiyo utapata na kidole chako, hata ukiwa na ile picha ya Mtukufu Rais hapo, bei ni hiyo hiyo. Kwa hivyo hakuna maana kuwa kwa KANU. Hata ukitingiza kidole mara kumi, bei haitapunguzwa.

Bw. Naibu Spika wa Muda, nazungumzia habari ya kodi. Pengine mhe. Mbunge yule hakusoma hii habari. Mimi husoma halafu na quote. Itamchukuwa miaka 28 ndipo ajue kusoma Bills. Katika Clause 38, ukurasa 204, wanasema kama ufuatavyo:

"Section 167 of the Customs and Excise Act is amended in subsection (4) (a) by deleting the word "twenty" and inserting the words "one hundred".

Zamani, katika hiyo Act, ilikuwa ni 20, lakini sasa imepelekwa mpaka 100. Ukifanya hesabu utajua umeongezwa nini. Sisi tutapitisha sheria hii kwa sababu wakati wa kupiga kura utaona upande huu umejaa "NOES" na "AYES" itaanguka hapa, na hata fisi, akiwa karibu atakimbia sana mpaka Nakuru kwa sababu ile kelele itakayovumwa ni nyingi. Lakini hawajui wanapitisha sheria ya kwenda kuwaumiza wale waliowachagua.

Bw. Naibu Spika, wa muda, kwenye ukurasa wa 206, Clause 51, wanaongea juu ya Permanent Secretaries and Judges. Hapa ndipo mimi nataka maelezo kutoka kwa Waziri wa Fedha. Wote hawako hapa. Waziri mwenyewe hayuko hapa, na Waziri msaidizi alikuwa hapa lakini akatoka. Alikuwa akisinziasinzia. Alikuwa na usingizi lakini akaenda kutembea kidogo.

"35. *Permanent Secretaries and Judges*

One motor vehicle (excluding buses and mini-buses of more than 13 passengers and load carrying vehicles of a load carrying capacity exceeding two tonnes) imported or purchased prior to clearance through customs by a Permanent Secretary or a Judge, subject to the written recommendation of the Permanent Secretary, Secretary to the Cabinet and Head of the Civil Service in the case of a Permanent Secretary and the Chief Justice in the case of a Judge.

Provided that the exemption under this item shall apply only once in every four years.

Sasa Bw. Naibu Spika wa Muda, umesikia kwamba vitu vinaingia bila kutozwa ushuru. Makatibu wa Kudumu wanafanya jambo hili. Kwa nini wanafanya hivi? Even if it applies to the Members of Parliament it should not happen. Mimi ningetaka Kamati ya Fedha ya Bunge iwe ikifanya kazi kwa sababu Serikali haiwezi kufanya kazi bila pesa. Tumesikia mengi kuhusu hawa makatibu wa kudumu. Hasa mimi niko very allergic kwa Makatibu wa Kudumu. Pesa zimeibiwa hapa katika Benki Kuu na hata ukisoma Ripoti ya Public Accounts Committee unaweza kulia machozi ya damu. Utasikia vile Makatibu wa Kudumu wanavyofyonza umma huu. Ningependa Kamati ya Fedha ya Bunge hili ifanye kazi yake. Hiyo ndiyo kazi tumepatiwa kufanya. Waheshimiwa wanafanya kazi gani? Hata hawakai Bungeni na hali wanalipwa. Wanakuja dakika mbili na wanapata mshahara wa mwezi mzima. Haki iko wapi kwa jambo kama hili? Hata kwa Mungu utaulizwa maswali kwa sababu Mungu amesema lazima utoke jasho ili ule. Sasa wewe unakuja dakika chache halafu unakwenda mahali unapotaka na Bunge linabaki tupu na hali mwisho wa mwezi unachukua mshahara. Kazi ndiyo hii ya Wabunge? Kazi yao ni kuchunga fedha na kodi ya wananchi. Wanastahili kuwa hapa kila mara ili wafanye kazi. Kamati zilizochaguliwa zifanye kazi. Tunataka ile Nyumba ya County Hall irekebishwa upesi ili hizi kamati zote zifanye kazi. Every Ministerial Committee must function. Kufuatana na Standing Orders kila Wizara inafaa iwe na Ministerial Committee. Huu ni wajibu wa hawa waheshimwa watukufu kufanya kazi na sio kukimbiakimbia na kuomba pesa. Hapo ndipo mambo yanaharibika. Na ajabu ni kuwa hawa waheshimiwa pia wana watoto na wajukuu.

An hon. Member: Harambee ifanyike.

Mr. Shikuku: Bw. Naibu Spika wa Muda, ninamsikia yule kijana akisema lazima Harambee ifanyike. Mnaibia wananchi halafu mnawaambia wafanye Harambee. Hiyo ni kuwafilisi. Kama kodi ingekuwa inalindwa hivi vitu vyote vingefanyika na Harambee ingekuwa kidogo. Lakini kwa sababu fedha zinapatikana na zinaliwa wananchi wanaambiwa wafanye Harambee. Juzi tu Mbunge wa Nakuru aliambiwa afanye Harambee ili angalie habari ya vyoo kule Nakuru. How do you do that? Mhe. aonekane kule Nakuru anafanya Harambee ya kufagia mavi vyooni na watu wanatoa service charge.

The Temporary Deputy Speaker (Mr. Wetangula): Use decent language, hon. Shikuku.

Mr. Shikuku: Bw. Naibu Spika Wa Muda, sijui Kiswahili kizuri ni kipi lakini hiyo ndiyo ninafahamu. Choo zifanyiwa Harambee!

The Temporary Deputy Speaker (Mr. Wetangula): Sema kinyesi.

Mr. Shikuku: Hata kikiwa kinyesi ni hali hiyo tu.

Bw. Naibu Spika wa Muda, hii ni aibu kubwa kumuuliza Mbunge kufanya Harambee, kufagia vyo ambavyo vimejaa na kodi inatolewa na inaliwa. Nchi hii imetoka kwa reli na sasa iko mchangani kwa shauri ya hawa waheshimiwa. Inaelekea kwenye hatari na hiyo hatari inaweza kumfanya mtu amwona Mungu kabla ya saa yake kufika. Na ukipata kuonana na Mungu na mambo yako ni maovu namna hii hali yako itakuwa mbovu sana.

Ukiangalia Clause 35 utapata wanasema:-

"Provided that exemption under this item shall only apply once in every four years."

Hapo chini wanasema yafuatayo:-

"(d) By deleting paragraphs (1),(2),(3),(4) and (5) of item 8 inserting the following:- (1) Household, personal effects of any kind imported by entitled personnel or their dependants including one motor vehicle imported or purchased by them prior to the clearance through Customs within 90 days of the first arrival in Kenya, or such longer period, not exceeding 360 days from the date of his arrival, as maybe approved by the Treasury in specific cases, where entitled personnel have not been granted an exemption under 7(3) of part A, or item 8(3) of part B of this Schedule."

